*Kioo cha Lugha, Juz. 22(1), 20-35*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam* **DOI:** https://dx.doi.org/10.4314/kcl.v22i1.2

# Ruwaza ya Kiidadi katika Ufafanuzi wa Vidahizo vya Kiantonimu katika Kamusi: Tathmini ya Kamusi Teule

*Jeremiah S. Andrew*[1] *na Mussa M. Hans*[2]

## Ikisiri

Maana za vidahizo katika kamusi huelezwa kwa kutumia mbinu mbalimbali. Miongoni mwa mbinu hizo ni matumizi ya antonimu ambazo hutumika zaidi kufafanua vidahizo vya kamusi za lugha moja kwa sababu walengwa wake huhitaji kupata maana kamilifu zote zinazotafutwa. Kwa msingi huo, antonimu zote zinazohusu kidahizo hutakiwa kuingizwa katika kidahizo husika kwa kufuata utaratibu. Ujitokezaji wa antonimu katika kamusi sio wa kiholela bali huzingatia uhusiano wa kimaana kati ya kidahizo na antonimu husika. Uhusiano huo ndio huamua idadi na aina ya antonimu zinazopaswa kuambatana na kidahizo, hivyo, kuunda ruwaza fulani ambazo huitwa ruwaza za kiidadi. Kuwapo kwa ruwaza hizo kumechangia kufanyika kwa utafiti huu unaotathmini kujitokeza kwa ruwaza za kiidadi katika ufafanuzi wa kiantonimu wa vidahizo vya kamusi wahidiya za Kiswahili. Nadharia Jumuishi ya Leksikografia imetumiwa katika uchambuzi wa data za makala hii. Data za zilikusanywa kutoka katika *Kamusi Kuu ya Kiswahili* toleo la tatu (yaani KKK3) kwa kutumia mbinu ya uchambuzi wa matini. Jumla ya vidahizo 379 vimebainika kutumia antonimu katika ufafanuzi wake na kuunda ruwaza tano za kiidadi zinazohusu umoja, uwili, utatu, unne na utano kutegemea idadi ya antonimu zilizotumika kuvifafanua vidahizo husika.

## 1.0 Utangulizi

Uhusiano wa kifahiwa ni miongoni mwa mambo yanayoshughulikiwa katika kamusi. Uhusiano huo huweza kuwa wa kiantonimia, kihomonimia, kipolisemia na kisinonimia. Makala hii imeushughulikia uhusiano wa kiantonimia ambao huukiliwa na matumizi ya antonimu. Antonimu ni neno au maneno yenye maana ya kinyume cha neno au maneno mengine (Cruse, 1986; Jones, 2002; Murphy, 2003; Jackson, 2013). Katika muktadha wa kamusi, antonimu hubeba pande mbili.

[1] Mhadhiri Msaidizi, Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania. Baruapepe: meshaluck@gmail.com
[2] Mhadhiri Mwandamizi, Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania. Baruapepe: mussahans30@gmail.com

Kwanza ni upande wa neno linalofasiliwa na pili ni neno linalofasili. Neno linalofasiliwa huitwa kidahizo ilhali neno linalofasili kwa kinyume huitwa antonimu. Antonimu moja au zaidi huweza kueleza maana ya kidahizo kimoja kutegemeana na uhusiano wa maneno hayo. Kidahizo husika kinapoingizwa katika kamusi hutakiwa kuambatana na antonimu zake ili kumsaidia mlengwa wa kamusi kuelewa zaidi uhusiano wa maneno yaliyopo katika lugha (Paradis na Willners, 2006). Kidahizo kimoja kinaweza kuwa na antonimu moja, mbili au zaidi kutegemeana na dhana inayorejelewa. Kuwapo kwa idadi hiyo ya antonimu zinazowekwa kwenye kidahizo kinachofafanuliwa ndiko kunakounda ruwaza ya kiidadi. Baadhi ya watungaji wa kamusi za jumla huingiza antonimu zote zinazohusiana na kidahizo husika ilhali baadhi yao huchagua chache tu na wengine huziacha kabisa.

Katika kamusi maalumu za antonimu, watungaji wa kamusi hujaribu kuingiza antonimu zote zinazohusu kidahizo kinachotomewa. Uingizaji huo kwa ujumla wake husababisha kuwapo kwa idadi tofautitofauti za antonimu ndani ya kamusi moja. Kuwapo kwa idadi hizo hutegemea mambo mbalimbali kama vile malengo ya kamusi, sifa za walengwa au wateja wa kamusi, aina ya vidahizo vilivyoingizwa, muda na bajeti ya mradi husika. Kujitokeza kwa antonimu hizo huweza kutofautiana kati ya kamusi moja na nyingine hata kama vidahizo havijabadilika. Utafiti wa awali ulionesha kwamba hakuna maandiko yanayoeleza kujitokeza kwa antonimu katika ufafanuzi wa vidahizo mbalimbali vya KKK3. Ukosefu wa maandiko hayo husababisha upungufu wa maarifa ya kileksikografia yanayohitajika kuboresha kamusi za lugha hii. Kwa msingi huo, tunaona kuna haja ya kuongeza maandiko kwa kuipambanua ruwaza ya kiidadi ilivyojitokeza katika KKK3.

Ruwaza ni mpangilio maalumu wa kitu au jambo unaoonesha kuzingatia urari mahususi (TUKI, 2019). Katika muktadha wa makala hii, ruwaza ni namna ambavyo antonimu zimejitokeza kiidadi katika ufafanuzi wa vidahizo mbalimbali vya kamusi. Antonimu hizo zinaingizwa kwenye kamusi ili kurahisisha kueleweka kwa maana za vidahizo husika. Matumizi ya antonimu katika kamusi husababisha kujitokeza kwa ruwaza mbalimbali kwa kuzingatia vigezo vya kiidadi, kimuundo, kimofolojia au kietimolojia (Murphy, 2003). Kigezo cha idadi ya antonimu huonekana bora zaidi kwa sababu hakimfungi mtafiti kuchunguza vipengele vyote vya kiisimu vinavyozihusu fahiwa zilizokusudiwa. Kwa mtazamo huu, ruwaza ya kiidadi ni jumla ya antonimu zilizotumika kufafanua kidahizo husika katika kamusi moja (Lobanova, Tom na Jeniffer, 2010). Ruwaza hizo huweza kupatikana kwa kuzingatia sifa za kidahizo jinsi kinavyofafanuliwa kiunyume. Hivyo, idadi ya antonimu inayobebwa huweza kuwa ya umoja (kidahizo kimoja kwa antonimu moja), uwili (kidahizo kimoja kwa antonimu mbili), utatu (kidahizo kimoja kwa antonimu tatu), unne (kidahizo kimoja kwa antonimu nne) au utano (kidahizo kimoja kwa antonimu tano au zaidi).

## 2.0 Ufafanuzi wa Dhana za Msingi Zilizotumika katika Makala

Katika makala hii zipo dhana za msingi zilizotumiwa. Dhana hizo ambazo zinatokana na mada ya utafiti, zimefafanuliwa ili kuiweka wazi mada iliyochunguzwa na kuonesha mipaka ya kimatumizi kulingana na makala hii. Dhana hizo ni antonimu, kidahizo na kitomeo.

### 2.1 Dhana ya Antonimu

Mazungumzo ya kila siku huwa na vitu viwili vyenye asili ya ukinzani na kushadadia dhana ya uwili katika matumizi ya lugha. Ukinzani wa kiuwili aghalabu ndio huzaa antonimu katika lugha. Kimsingi, antonimu ni neno lenye maana husiani ambayo ni kinyume cha neno jingine. Kutokana na mtazamo huo, wataalamu hufafanua antonimu kama aina ya maneno katika lugha yanayozalisha maana zinazopingana (Murphy, 2003; Habwe na Karanja, 2012; Kahigi, 2019). Kwa mfano; 'nzuri #[3] **mbaya**', 'tajiri # **maskini**', 'nawiri # **fubaa**'**.** Katika mifano hii, maneno ya kila jozi huchukuliwa kama antonimu ya neno jingine. Katika muktadha wa kamusi, neno linaloingizwa kama kidahizo, licha ya kubeba sifa ya uantonimu, huwa halichukuliwi kama antonimu isipokuwa tu kama litatumika kufafanua kidahizo kingine. Kwa msingi huo, maneno yenye hati iliyokoza tu ndiyo yanapaswa kuitwa antonimu za vidahizo husika ingawa kimantiki pande zote huingiliana na kubadilika kiuhusiano. Maneno haya yamechukuliwa kuwa ndizo antonimu kwa sababu kimpangilio huwa yamewekwa kwenye ufafanuzi wa kidahizo.

Vilevile, antonimu hurejelea mkinzano wa kimaana kwa neno moja kubeba maana tofauti na neno jingine. Maana zinazobebwa huwa ni unyume baina ya maneno husika ambayo huweza kubadilishana nafasi katika tungo. Maneno hayo hubadilishana nafasi kiuamilifu ili kukidhi maana na kusudi la tungo husika (Baker, 2001). Kuna antonimu za aina nyingi kutegemea vigezo vya kisemantiki, kimofolojia, kietimolojia na kidhima (Gibbe, 1977; Cruse, 1986; Habwe na Karanja, 2004; Geeraerts, 2010; Kahigi, 2019). Aidha, kwa kuzingatia kigezo cha kisemantiki, ambapo leksikografia hupatikana humo, uainishaji wa antonimu huhusu makundi ya kiukamilishani, kimuelekeo, kimakadirio na kiukinzani. Kwa mfano, Kahigi (2019) anaainisha antonimu katika makundi ya ukamilishani, ukadirifu, uelekeani na utenduzi kama inavyofafanuliwa katika aya zinazofuata.

Antonimu kamilishani hutokana na uhusiano wa maneno ambayo kuwapo kwa neno moja husababisha kuwapo kwa neno jingine linalounda maana inayohitaji kukamilishwa. Neno linalokosekana ndilo hufumbata maana ya neno lililotajwa kwa sababu maneno hayo huwa hayawezi kutokea mahali pamoja au kutumiwa yote kwa pamoja. Kahigi (2019) anasema kwamba antonimu kamilishani huwa na mipaka isiyopitika; yaani, antonimu moja inapokanushwa huwa inaneneleza kinyume

[3] Katika makala hii msimbo # umetumika kuonesha antonimu yaani '*kinyume cha*'

chake. Kahigi anatumia mifano kama vile, ‘*-fu # hai*’, ‘*kweli # sikweli*’ na ‘*endelea # acha*’.

Aina nyingine ni antonimu za kimuelekeo. Haya ni maneno ambayo uhusiano wake wa kimaana huashiria mijongeo fulani kutoka kituo kimoja kwenda kingine. Muktadha wa kimatumizi katika antonimu hizi hujulikana kwa watumiaji wa lugha husika. Antonimu za kundi hili hujenga maana zake kupitia uzoefu wa watumiaji wa lugha husika kutambua kizio ambacho maneno husika huanzia kuchanuza maana zake; ambapo kwa kadiri yanavyoachana kwa uelekeo tofauti ndivyo maana zake za unyume hupatikana. Miongoni mwa mifano katika kundi hili inajumuisha seti za ‘*uza # nunua*’, ‘*juu # chini*’, ‘*kulia # kushoto*’ na ‘*kaskazini # kusini*’ (Kahigi, 2019).

Vilevile, kuna antonimu linganishi. Aina hii hutokana na maneno ambayo maana zake huzalishwa kwa kuzingatia viwango tofauti vya kiuwiano vinavyojazwa maneno hayo. Aghalabu, kipimo cha viwango huwa si bayana kwa kuwa huzingatia uzoefu wa kisemantiki walionao watumiaji wa lugha inayohusika. Antonimu hizi hujikita zaidi kwenye makadirio na neno moja tu ndilo hutumika kuuliza ama kuelezea kiwango cha makadirio ya sifa husika (Kahigi, 2019). Kundi hili hujumuisha antonimu zinazohusu maneno kama vile: ‘*kubwa # ndogo’*, ‘*-refu # -fupi’* na ‘*baridi # joto*’.

Pia, kuna antonimu za kiuhusiano ambazo hutokana na sifa za kiumiliki zilizopo katika maneno husika. Sifa hizo huwa haziwezi kutajwa au kutokea kwenye neno moja pasipo kudokeza neno jingine lenye udugu nalo. Antonimu za kiuhusiano huwa na tabia ya kurejeleana kwa sababu kuibuka kwa maana yake ni lazima kudokezwe kwa kuzingatia udugu wa kiisimu. Mifano ifuatayo inadhihirisha hali ya uhusiano wa kurejeleana: ‘*mwajiri # mwajiriwa’, ‘mzazi # mtoto’.*

## 2.2 Kidahizo

Kidahizo ni neno linaloingizwa katika kamusi aghalabu kwa chapa iliyokoza au rangi nyingine kisha kutolewa ufafanuzi (Zgusta, 1971; Mdee, 2010). Kidahizo ni neno kuu katika kamusi kwa sababu ndicho huamua taarifa za kisarufi, kifonolojia, kisemantiki, kimofolojia na kipragmatiki zinazopaswa kuwapo katika kitomeo. Kidahizo ni moyo wa kamusi yoyote kwa sababu ndicho hutafutwa na walengwa wa kamusi. Katika kamusi za lugha moja, kidahizo na ufafanuzi hutolewa kwa lugha moja.

## 2.3 Kitomeo

Kitomeo ni kidahizo kilichoingizwa katika kamusi pamoja na ufafanuzi wake. Ufafanuzi huo mara nyingi ndio huhitajiwa na mlengwa wa kamusi (Mdee, 2010). Ufafanuzi wa kidahizo hujumuisha taarifa kama vile matamshi, fasili, mifano ya matumizi, sinonimu, antonimu na vielelezo vinavyosaidia kueleweka kwa maana ya kidahizo. Kitomeo huchukuliwa kama aya ya kileksikografia ambayo huwa ndio uti wa mgongo wa kamusi husika. Aghalabu kitomeo huukilia mwonekano na maudhui

ya kamusi iliyotungwa kutegemea taarifa za kidahizo zilizoingizwa katika ufafanuzi. Taarifa hizo hutegemea kategoria ya kidahizo husika na malengo ya kamusi hiyo. Utambuzi wa vitomeo umesaidia kubainisha antonimu mbalimbali zilizohusika katika ufafanuzi wa vidahizo vya KKK3.

**3.0 Methodolojia na Nadharia ya Utafiti**

Data za makala hii zimekusanywa maktabani kwa kutumia mbinu ya usomaji wa matini. Chanzo cha data ni KKK3 iliyotungwa na Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) mwaka 2022. Baada ya kuipitia matini hiyo yenye vidahizo 22,675, ilibainika kwamba vidahizo 379 vimetumia antonimu kufafanua maana zake. Aidha, umahususi uliwekwa katika vidahizo 379 vyenye ufafanuzi wa kiantonimu. Vidahizo hivi vilichunguzwa na kuchambuliwa kimaudhui na kiulinganishi ili kupata idadi ya antonimu zilizoingizwa katika kila kitomeo cha alfabeti za Kiswahili kuanzia herufi A-Z. Hata hivyo, herufi 'Y' ilibainika kutotumia kabisa antonimu kufasili vidahizo vyake. Idadi ya antonimu imedokeza ruwaza za kiidadi zilizojitokeza kwenye KKK3. Vidahizo na antonimu zake zimeteuliwa kinasibu kutoka kwenye kila ruwaza ili kuwasilisha data nzima iliyokusanywa maktabani. Makala hii imetumia sampuli ya vidahizo 17 kama majedwali Na.1-5 yanavyoonesha. Vidahizo hivyo vilitumika kulingana na uhitaji wake katika kushadidia hoja zilizotolewa kuhusu ruwaza za kiidadi katika ufafanuzi wa vidahizo kiantonimu. Mgawanyo wa sampuli ya vidahizo kwa kila ruwaza ni: 6 kwa ruwaza ya umoja, 3 kwa ruwaza ya uwili, 2 kwa ruwaza ya utatu, 3 kwa ruwaza ya unne na 3 kwa ruwaza ya utano. Ruwaza za kiidadi katika KKK3 zimetokana na antonimu zilizotumika kwenye kila ufafanuzi wa kidahizo. Katika uwasilishaji hoja na uchanganuzi wa data, mbinu ya uhakiki ilitumika kwa kutathmini muundo unaoweza kuimarisha zaidi maana za vidahizo vya unyume katika KKK3. Tathmini hizo zimetokana na aina ya taarifa za kiantonimu zilizoingizwa kwenye ufafanuzi wa vidahizo husika. Taarifa zilizoingizwa ni pamoja na idadi ya antonimu za kidahizo husika, urejeleano wa kimaana na asili ya antonimu iliyopo kuwa na neno jingine linalobeba maana yake ya kiusawe.

Aidha, makala hii imeongozwa na Nadharia Jumuishi ya Leksikografia iliyoasisiwa na Herbert Wiegand mwaka 1970. Nadharia hii ilianzishwa ili kueleza kanuni za jumla za leksikografia zinazohusu utungaji, upitiaji na uhakiki wa kamusi mbalimbali. Nadharia hii inajumuisha pia suala la kuzingatia kipengele cha uamilifu wa kileksikografia unaokidhi mahitaji ya mlengwa wa kamusi husika. Uamilifu wa kileksikografia unasaidia kutambua thamani ya kila data na kila kipengele kinachoingizwa katika kamusi husika ili kutompotosha mlengwa wa kamusi husika. Kimsingi, nadharia hii inadokeza masuala yanayopaswa kufuatwa wakati wa kutunga na kuhakiki kamusi ili kuwakutanisha kileksikografia mtungaji na mlengwa wa kamusi husika. Pia, inamwelekeza mhakiki kufuata mambo muhimu anapoipitia na kuihakiki kamusi husika. Mawazo ya nadharia hii yamejumuishwa katika misingi miwili ifuatayo:

Mosi, msingi unaosisitiza kutunga kamusi kwa kuzingatia mahitaji ya walengwa wa kamusi husika. Msingi huu unajikita katika kumwondolea shaka mlengwa wa kamusi husika juu ya maneno na taarifa zote anazotegemea kuzikuta ndani ya kamusi. Taarifa zinazohitajiwa na mtumiaji ni muhimu zipatikane waziwazi katika kamusi husika ili kurahisisha ujifunzaji wa kipengele mahususi kinachokusudiwa. Kwa mujibu wa msingi huu, watungaji wa kamusi ni lazima waingize taarifa zote za kisarufi na kileksikografia zinazohusu kidahizo husika. Upungufu wa taarifa hizo unaweza kuwapo kama mwongozo wa mtumiaji umedokeza tahadhari hiyo. Msingi huu ulisaidia kutambua ruwaza za kiidadi zilizotawala zaidi katika ufafanuzi wa vidahizo kwa kutumia antonimu.

Pili, msingi unaohimiza watungaji wa kamusi kuzingatia matumizi ya nadharia za taaluma zingine zinazohusiana na kamusi inayotungwa. Nadharia hizo huhusu taaluma za mofolojia, fonolojia, sintaksia, semantiki, teminografia na lugha kwa ujumla. Pia, zinaweza kuwapo nadharia za nje ya isimu kama vile sheria, takwimu na utamaduni. Kinachosisitizwa ni matumizi sahihi ya nyanja zingine zinazoikamilisha kamusi husika. Katika uchambuzi wa data, idadi ya antonimu katika ufafanuzi wa kila kidahizo ilikuwa ndiyo mwongozo wa kuamua aina ya ruwaza. Msingi huu umetuongoza kuhakiki matumizi ya maarifa ya kitakwimu kwa kuhesabu idadi ya antonimu zilizoingizwa katika kila kidahizo chenye ufafanuzi wa kiantonimu.

## 4.0 Ruwaza za Kiidadi katika Antonimu za KKK3

Mtungaji wa kamusi hutarajiwa kuingiza maneno yenye sifa za kuunda maana ya kinyume katika kitomeo husika (Paradis na Willners, 2006). Kwa kuwa maneno hutofautiana kiuhusiano, idadi ya antonimu kwa kila kidahizo huweza kutofautiana. Hata hivyo, mahitimisho ya mwonekano wa kamusi nzima ndiyo hudhihirisha kuwa kamusi imetumia ruwaza gani na kwa kiwango gani. Ruwaza kuu tano za kiidadi zimejitokeza katika KKK3 kama zilivyojadiliwa katika vipengele vinavyofuata.

### 4.1 Ruwaza ya Kidahizo Kimoja kwa Antonimu Moja

Ruwaza ya kidahizo kimoja kwa antonimu moja hujulikana pia kama ruwaza ya umoja. Katika vitomeo vyote vya aina hii, antonimu moja tu ndiyo hutumika kufafanua maana ya kidahizo husika. Aghalabu, ruwaza hii inapojitokeza husababisha watungaji wa kamusi kuingiza antonimu kama kidahizo huru ili kupanua uwezekano wa kueleweka zaidi kwa maana ya maneno yanayohusika. Matokeo ya utafiti yamebaini kuwa KKK3 ina vidahizo 261 kati ya 379 ambavyo ni sawa na 68.87% vilivyotumia ruwaza ya umoja kwa kuingiza antonimu mojamoja. Katika ruwaza hii kuna antonimu zilizoingizwa moja kwa moja ili kuonesha kinyume cha kidahizo husika. Pia, zipo antonimu zilizotajwa na kuingizwa kimantiki katika ufafanuzi wa kidahizo. Tuchunguze Data Na. 1 inayohusu kidahizo ‘dosari’ na antonimu yake ‘ukamilifu’ iliyoingizwa moja kwa moja kwa kubainishwa kuwa ni kinyume cha kidahizo.

1. **dosari** */dɔ'sari/ nm.*(Ø) {*i-/zi-*} upungufu wa kukosa utimilifu katika mwili au jambo ***vis.:*** kasoro, walakini, hitilafu ***kiny.:*** ukamilifu ►Kiar.

   **Chanzo:** BAKITA (2022: 173)

Aidha, katika Data Na. 2 yenye kidahizo 'bahasa' antonimu 'gharama' imeingizwa kimantiki pasipo kutumia kibainishi '**kiny.**' kama ilivyotajwa kwenye mwongozo wa mtumiaji wa KKK3. Hapa maarifa ya kisemantiki yametumiwa kuipambanua antonimu ambayo imetumika kama msingi wa ujenzi wa maana ya kidahizo husika.

2. **bahasa** */ba'hasa/ kiv.* –siyouzwa kwa gharama kubwa; -a bei ndogo; bwerere ►Kiar. **Chanzo:** BAKITA (2022: 51)

Katika Data Na. 1 na 2 imebainika kuwapo kwa antonimu moja inayofafanua zaidi maana za vidahizo husika. Matumizi ya antonimu moja katika ufafanuzi yamezingatia kanuni ya kisemantiki ya kuepusha mrundiko wa antonimu kwenye kidahizo kimoja. Hali hii hurahisisha upatikanaji wa maana isiyomzungusha mtumiaji wa kamusi husika. Idadi hii imetumika katika mazingira ya kidahizo kuwa na antonimu zaidi ya moja na vile vyenye antonimu moja tu ilibidi itumike hiyohiyo kwa kidahizo chenye uhitaji wa ufafanuzi wa kiunyume. Mtungaji wa kamusi huamua kuiteua antonimu moja tu ili kupata umbo la wastani la kamusi husika kwa kujali uwekevu wa nafasi. Aghalabu, vigezo vya uteuzi huwa ni mdafao wake wa kimatumizi na hali ya urejeleano. Tuchunguze mfano wa ruwaza hizo katika Jedwali Na. 1.

**Jedwali Na.1: Ruwaza ya Kidahizo Kimoja kwa Antonimu Moja**

| Na. | Kidahizo | Antonimu |
|---|---|---|
| 1. | bahasa | ghali |
| 2. | dosari | ukamilifu |
| 3. | sasa[1] | baadaye |
| 4. | uchechefu | wingi |
| 5. | wingi[1] | uchache |

**Chanzo:** BAKITA (2022)

Jedwali Na. 1 linaonesha ruwaza ya umoja kwenye ufafanuzi wa unyume katika vidahizo vya KKK3. Vidahizo vinavyohusika katika ruwaza hiyo hutokana na kamusi husika kuingiza antonimu moja tu kwenye vidahizo vilivyobeba sifa ya unyume. Kuwapo kwa antonimu mojamoja kumethibitika kutawala sehemu kubwa ya ruwaza za kiidadi katika KKK3. Kujitokeza kwa ruwaza hii kunaashiria kuwa maneno mengi (68.87%) katika KKK3 yana uhusiano wa kinyume kwa neno mojamoja au hata inapotokea yapo zaidi ya moja basi moja ndilo hutawala kimatumizi. Hata hivyo, licha ya uwiano huu wa kiruwaza, baadhi ya vidahizo vinaonekana kunyimwa antonimu zake zingine. Kwa mfano, ***wingi*** limepewa

antonimu moja tu *'uchache'* ila katika kidahizo cha ***uchechefu*** kuna antonimu *'wingi'*. Kutokana na Jedwali Na. 1, tuchunguze Data Na. 3 na 4 kwa ufafanuzi zaidi.

3. **wingi**[1] */`wiŋgi/ nm.* (Ø) {*u*-} hali ya kitu au kiumbe kuwapo kwa idadi kubwa; kinyume cha uchache.
   **Chanzo:** BAKITA (2022: 1143)

4. **uchechefu** */uʧɛ`ʧɛfu/ nm.* (Ø) {*u*-} uchache au udogo wa kitu; uhaba ***vis.:*** akali, ukalili ***kiny.:*** wingi
   **Chanzo:** BAKITA (2022: 1018)

Kwa kuwa kamusi haikubainisha aina za antonimu zilizoingizwa, ingefaa kama KKK3 ingezijumuisha antonimu zote husianifu katika kidahizo chake ili kutomchanganya mlengwa wa kamusi hiyo. Hapa kidahizo ***wingi*** kingeweza kujumuisha antonimu 'uchache' na 'uchechefu' ambazo hudokeza unyume wa kidahizo husika kutegemea muktadha na mada ya matumizi.

Pia, vidahizo vingine vimepewa antonimu zenye maana fiche. Ufiche na ufinyu wa maana huweza kusababishwa na ukosefu wa baadhi ya taarifa za kiantonimu ambazo zingefaa kuipambanua zaidi maana ya kidahizo kinachohusika. Kukosekana kwa antonimu husika kunaweza kupunguza uzito wa maana iliyopaswa kumfikia mlengwa wa kamusi. Tuchunguze Data Na. 5 inazohusu kidahizo 'sasa' jinsi kilivyofafanuliwa kwa antonimu 'baadaye' ambayo imeoneshwa katika Data Na. 6.

5. **sasa**[1] */`sa:sa/ kiel.* wakati uliopo; muda huu **mat.:** *Ndege imewasili ~.* ***kiny*.:** baadaye ► Kiar.
   **Chanzo:** BAKITA (2022: 885)

6. **baadaye** */baa`da:jɛ/ kiel.* wakati au muda wowote ujao kuanzia sasa **mat.:** *tutaonana ~.* ***kis*.:** halafu ►Kiar.
   **Chanzo:** BAKITA (2022:44)

Data Na. 5 na 6 zinaonesha kwamba ufafanuzi uliotolewa katika kidahizo 'sasa[1]' na 'baadaye' haudadavui kwa undani pande zote zinazohusu kabla na baada ya wakati kutokea. Kwa kurejelea Data Na. 5, kidahizo 'sasa[1]' kimepewa antonimu moja ilhali ilipaswa kuwekewa antonimu zaidi ya moja zinazoendana na uelekeo wa nyakati za unyume, yaani wakati uliopita na ujao. Mtumiaji wa KKK3 anapaswa kuzingatia tahadhari ya kuchagua vidahizo husika na antonimu zake kutegemea muktadha wa matumizi pamoja na mada ya mawasiliano. Kimsingi, matumizi ya antonimu mojamoja yamesaidia kuipata kamusi yenye saizi ya wastani inayoweza kubebeka kirahisi kwa walengwa wake ingawa katika vidahizo vichache (118/379), zimeingizwa antonimu zaidi ya moja katika ufafanuzi wa kila kidahizo.

### 4.2 Ruwaza ya Kidahizo Kimoja kwa Antonimu Mbili

Katika makala hii, ruwaza ya uwili ni ufafanuzi wa vidahizo kwa kutumia antonimu mbili tu. Imebainika kuwa KKK3 ina ruwaza ya uwili ambapo kidahizo kimoja kimefafanuliwa kwa antonimu mbili zinazodokeza maana ya kidahizo husika kwa kinyume. Antonimu zote mbili zinazojitokeza katika ruwaza hii sharti ziwe na sifa ya usawe miongoni mwazo. Katika vidahizo 379 vilivyotumia antonimu kufafanua maana zake, kuna vidahizo 92 ambavyo ni sawa na 24.27% vyenye ruwaza ya uwili. Katika ruwaza hiyo, antonimu ya kwanza na ya pili huweza kubadilishana nafasi katika mpangilio wake kwenye kamusi husika ingawa sio lazima ziunde maana iliyo sawa (visawe kamili). Kinachozingatiwa zaidi ni hali ya antonimu hizo kukubalika zaidi katika lugha husika pamoja na hali ya urejeleano wa leksimu zinazohusika kuunda maana ya kidahizo. Jedwali Na. 2 linaonesha mfano vidahizo vilivyofafanuliwa kwa kutumia antonimu mbilimbili.

**Jedwali Na. 2: Ruwaza ya Kidahizo Kimoja kwa Antonimu Mbili**

| Na. | Kidahizo | Antonimu 1 | Antonimu 2 |
|---|---|---|---|
| 1. | abu | nina | mama |
| 2. | ghasia | utulivu | usalama |
| 3. | vita | amani | utulivu |

**Chanzo:** BAKITA (2022)

Jedwali Na. 2 linaonesha ruwaza ya uwili ya antonimu za KKK3. Katika ruwaza hiyo antonimu zilizoingizwa kueleza maana ya kidahizo zinahusiana na kuelekeana kidhana. Uhusiano wa antonimu hizo huwa siyo lazima uunde maana sawa kabisa katika maneno hayo. Tuchunguze Data Na. 7 na 8 kwa ufafanuzi zaidi.

7. **abu** */`a:bu/ nm.* (*Ø*) {*a-/wa-*} (*kish.*) mzazi mwanaume ***kis.:*** baba ***viny.:*** nina, mama ►Kiar. **Chanzo:** BAKITA (2022: 3)

8. **nina** */`nina/ nm.* (*Ø*) {*a-/wa-*} mzazi kike ***kis.:*** mama. **Chanzo:** BAKITA (2022: 777)

Data Na. 7 inaonesha antonimu ‘nina’ na ‘mama’ zilivyotumika kufafanua kidahizo ‘abu’ ilhali Data Na. 8 inaonesha kuwa ‘mama’ ni kisawe cha kidahizo ‘nina’. Kwa hiyo, maana zinazojengwa na antonimu za kidahizo kimoja huhusiana na kuwa visawe. Pamoja na kwamba antonimu hizo hufanana kimaana, zinaweza kutofautiana ama kuachana kimaana kutegemea uzito wa kiuhusiano na kidahizo husika. Kutokana na mwachano huo wa kidhana, baadhi ya walengwa wa kamusi huweza kuamua kujiegemeza kwenye dhana moja tu inayoibuliwa na antonimu mojawapo.

Vilevile, baadhi ya vidahizo vya KKK3 vyenye antonimu mbili vilipaswa kuwa na antonimu zaidi ya mbili kutokana na maana yake ya msingi iliyofafanuliwa. KKK3 haijaonesha msingi wa kuamua idadi faafu kwa kila kidahizo chenye sifa ya antonimu. Tuchunguze Data Na. 9 kwa ufafanuzi zaidi.

9. **ghasia** */ɣa`sija/ nm.* (Ø) {*i-/zi-*} tukio la vurugu au fujo linalosababisha kutokuwapo kwa hali ya amani. ***vis.:*** machafuko, ugomvi, zahama, rabsha ***kiny.:*** utulivu, usalama ►Kiar.
**Chanzo:** BAKITA (2022: 241)

Katika Data Na. 9 kidahizo 'ghasia' kimefafanuliwa kwa antonimu mbili tu yaani *'utulivu'* au *'usalama*'. Kiasili kidahizo hiki kina antonimu zingine kama vile '*amani'*. Antonimu hii imeachwa ilhali inaweza kubeba dhana inayohusu kinyume cha kidahizo 'ghasia'. Kupungua kwa antonimu husika kumetokana na maamuzi ya watungaji wa kamusi kutoingiza antonimu zote za vidahizo vya KKK3 na siyo asili ya kidahizo chenye idadi kamilifu ya antonimu husika. Kimsingi, antonimu zote zinapaswa ziingizwe katika kidahizo husika ili mlengwa wa kamusi asitatizwe kuyapata maneno yote yanayohusiana na kidahizo husika.

### 4.3 Ruwaza ya Kidahizo Kimoja kwa Antonimu Tatu

Ruwaza ya kidahizo kimoja kwa antonimu tatu hujulikana pia kama ruwaza ya utatu ambapo kidahizo kimoja hufafanuliwa kwa kutumia vinyume vitatu. Katika lugha ya Kiswahili, baadhi ya maneno huwa na sifa ya kubeba antonimu tatu kutegemea dhana inayohusiana na maneno hayo. Sifa hiyo ya utatu imejitokeza pia katika KKK3. Antonimu zenye sifa hiyo huweza kuingizwa katika kamusi kwa namna kuu mbili. Mosi, neno mojawapo hutumika kufafanua kidahizo na mengine hulifuata kama sinonimu ya neno (antonimu) hilo. Pili, maneno yote matatu huingizwa kama antonimu ya kidahizo kinachofafanuliwa kwa kutumia vinyume. Imebainika kuwa vidahizo 13 kati ya 379 vilivyoingiziwa antonimu ili kufafanua maana zake katika KKK3 vimetumia ruwaza ya utatu. Ujitokezaji wa ruwaza hii ni sawa na 3.43%. Jedwali Na. 3 linaonesha baadhi ya vidahizo vyenye data za ruwaza ya utatu wa antonimu za KKK3.

**Jedwali Na. 3: Ruwaza ya Kidahizo Kimoja kwa Antonimu Tatu**

| Na. | Kidahizo | Antonimu 1 | Antonimu 2 | Antonimu 3 |
|---|---|---|---|---|
| 1. | **amani** | vita | vurugu | usumbufu |
| 2. | **mutlaki** | kizuizi | wasiwasi | shaka |

**Chanzo:** BAKITA (2022)

Jedwali Na. 3 linaonesha kuwa baadhi ya vidahizo vya KKK3 vimefafanuliwa kwa kutumia antonimu tatu ili kuboresha zaidi maana ya maneno hayo. Katika ruwaza ya utatu wa kiantonimu maneno hupangwa kutegemea namna yanavyotumika zaidi katika jamii. Maneno yanayotumika mara kwa mara ndiyo hupaswa kutangulia kuingizwa yakifuatiwa na mengine kwa kuzingatia kiwango cha ujitokezaji wake katika jamii inayotumia lugha husika. Aidha, antonimu za mtindo huu zina sifa ya kurejeleana kimaana na kidahizo husika, ambapo zenyewe kwa zenyewe huwa na

maana inayofanana lakini maana ya maneno hayo huwa ni kinyume na kidahizo. Tuchunguze Data Na. 10 na 11 kwa ufafanuzi zaidi.

10. **amani** */a`ma:ni/ nm.* (Ø) {*i-/zi-*} **a.** hali ya kuwapo kwa utulivu dhidi ya usumbufu **b.** hali ya kuwa na usalama na utulivu; kutokuwa na vita au vurugu yoyote **ch.** makubaliano ya usalama baina ya nchi zenye vita **Chanzo:** BAKITA (2022: 22)

11. **mutlaki** */`mutlaki/ kiv.* –isiyo na kizuizi wala masharti yoyote; -siyo na wasiwasi au shaka yoyote. **Chanzo:** BAKITA (2022: 724).

Kwa kuzingatia Data Na. 10 na 11 imebainika kwamba maana ya vidahizo vya KKK3 imefafanuliwa kwa kutumia antonimu tatu. Antonimu za ruwaza hii zimejitokeza kwa kufungamanishwa na vikanushi vinavyosaidia kuupambanua ufafanuzi husika. Mpangilio wa antonimu hizo unaakisi uhusiano wa kidhana uliowekwa kwenye kidahizo kinachofafanuliwa na antonimu husika. Licha ya kigezo cha kidhana, mpangilio wa antonimu hizo huweza kuzingatia kigezo cha kialfabeti ambapo huangalia zaidi herufi zinazounda neno husika. Antonimu hizo hazijaingizwa kiholela katika ufafanuzi wa vidahizo husika. Uingizaji usio holela husaidia kuyafikia mahitaji ya mlengwa wa kamusi kirahisi, kiasi cha kupatikana kwa maana zote zinazokihusu kidahizo kinachofafanuliwa.

### 4.4 Ruwaza ya Kidahizo Kimoja kwa Antonimu Nne

Ruwaza ya kidahizo kimoja kwa antonimu nne hujulikana pia kama ruwaza ya unne kwa sababu ufafanuzi wa kidahizo husika hutumia antonimu nne. Imebainika kuwa vipo vidahizo vya KKK3 vyenye ufafanuzi wa antonimu nne. Katika hali hiyo, maana ya kidahizo kimoja huweza kupatikana kwenye vinyume vya maneno manne tofauti. Antonimu zote nne zilizotumika katika ufafanuzi hukaribiana au hufanana kabisa kimaana. Kinyume cha maana ya maneno hayo hufumbata dhana iliyomo kwenye kidahizo kilichoingizwa katika kamusi. KKK3 ina vidahizo 9 kati ya 379 vilivyotumia ruwaza ya unne kuingiza antonimu katika kidahizo. Idadi hii ni sawa na 2.37%. Mtawanyiko wa ruwaza hii haujatumika kwenye herufi zote, hivyo, baadhi ya alfabeti kama vile ‘ch’, d’, ‘e’, ‘f’ na ‘j’ hazina kabisa uwakilishi wa antonimu za unne kwenye KKK3. Jedwali Na. 4 linaonesha baadhi ya vidahizo vilivyofafanuliwa kwa kutumia antonimu nnenne.

**Jedwali Na. 4: Ruwaza ya Kidahizo Kimoja kwa Antonimu Nne**

| Na. | Kidahizo | Antonimu 1 | Antonimu 2 | Antonimu 3 | Antonimu 4 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | **adimika** | tapakaa | enea | zagaa | shamiri |
| 2. | **hafidhina** | mwanausasa | mmamboleo | mwanamageuzi | mpenda mabadiliko |
| 3. | **uhafifu** | ukakamavu | uthabiti | uimara | ubora |

**Chanzo:** BAKITA (2022)

Jedwali Na. 4 linadokeza ruwaza ya unne wa antonimu zilizoingizwa katika KKK3. Antonimu zote zilizotumika kufafanua kidahizo hubeba maana ya unyume wa kidahizo ingawa huweza kutofautiana kimatumizi na kiuzito katika lugha husika. Tuchunguze Data Na. 12 kwa ufafanuzi zaidi.

**12. uhafifu** */uha`fi:fu/ nm.* **a**. hali ya kuwa na kiwango kidogo cha ubora ***mat.:*** *baadhi ya bidhaa zinazoingia nchini zimegundulika kuwa na ~.* ***kis.:*** uduni ***kiny.:*** ubora **b**. hali ya mtu au kitu kuwa na udhaifu; hali ya kukosa nguvu ***mat.:*** *siku hizi hapigani ngumi za kulipwa kwani mwili wake una ~* ***viny.:*** ukakamavu, uthabiti, uimara. **Chanzo:** BAKITA (2022: 1036)

Katika Data Na. 12 maana za kidahizo husika zimefafanuliwa zaidi kwa kujazilizwa antonimu nne. Antonimu moja imetumika katika fahiwa ya kwanza ilhali antonimu zingine tatu zimetumika katika fahiwa ya pili. Licha ya kutumika katika fahiwa mbili tofauti, ni dhahiri kuwa antonimu zote huweza kusimama katika darajia moja na kudokeza unyume wa kidahizo ‘uhafifu’. Aidha, kujitokeza kwa antonimu zaidi ya moja katika kidahizo kimoja kunatokana na uhusiano chanya wa antonimu uliofumbatwa katika maneno hayo. Uhusiano chanya wa antonimu za kidahizo kimoja husababisha antonimu hizo ziwe ni visawe zenyewe kwa zenyewe kwa sababu kwa ujumla wake huunda maana inayoelekeana. Maneno hayo yanayoelekeana kimaana hupaswa kuingizwa yote ndani ya ufafanuzi wa kidahizo husika. Kwa kurejelea Data Na. 12, maneno ‘ubora’, ‘ukakamavu’, ‘uthabiti’ na ‘uimara’ kila moja ni kisawe cha jingine.

Hata hivyo, maana ya antonimu zinazokifafanua kidahizo kimoja huweza kutofautiana kimatumizi kutegemea mada na muktadha wa mawasiliano. Kwa hiyo, mtumiaji wa kamusi hupaswa kuwa makini kuamua ni kinyume kipi hasa akirejelee anapowasiliana. Tuchunguze Data Na. 13 kwa ufafanuzi zaidi.

13. **adimika adimik.a** */a:di`mika/ kit. sie.* patikana kwa nadra au kwa shida sana ***kis.:*** kosekana ***viny.:*** tapakaa, enea, zagaa, shamiri ⇌ *adimika, adimikika, adimikisha* ►Kiar. **Chanzo:** BAKITA (2022: 7)

Katika Data Na. 13, antonimu za kidahizo **‘adimika’** ambazo ni ‘*tapakaa’*, ‘*enea’*, ‘*zagaa’* na ‘*shamiri’* zimetofautiana kidhana kwa kuwa sio sinonimu kamili. Tofauti za kidhana zilizobebwa na antonimu hizi humfanya mtumiaji wa kamusi kuangalia na kutumia maneno sahihi hasa visawe vya kidahizo vinavyoikubali mada na muktadha wa kinachojadiliwa. Matumizi sahihi ya antonimu hizi hutegemea kiwango alichonacho mlengwa wa KKK3 katika umilisi wa lugha ya Kiswahili. Licha ya tofauti ndogo za kimaana zilizopo katika antonimu za vidahizo vya kamusi madhukura, baadhi ya antonimu huwa na uzito sawa wa kimaana na huweza kubadilishana nafasi. Tuchunguze Data Na. 14.

14. **hafidhina** */hafi`ðina/ nm.* (*wa*-) {*a-/wa*-} pia **mhafidhina** mtu mwenye kushikilia mambo ya kale; mtu asiyependa mabadiliko ***viny.:*** mwanausasa, mmamboleo, mwanamageuzi, mpenda mabadiliko ►Kiar.
**Chanzo:** BAKITA (2022: 266)

Data Na. 14 inaonesha antonimu nne zilizoingizwa katika ufafanuzi wa kidahizo kimoja ilhali zenyewe kwa zenyewe zina hadhi sawa ya kuweza kutumika kimbadilishano. Antonimu zote nne zina muundo mwambatano na zinaweza kutumika katika mazingira yaleyale ya mawasiliano ya lugha ya Kiswahili. Kuwapo kwa antonimu zisizopishana sana kidhana humpa uhuru mlengwa wa KKK3 kuzitumia kwa namna mbalimbali pasipo kupoteza maana iliyokusudiwa.

### 4.5 Ruwaza ya Kidahizo Kimoja kwa Antonimu Tano au Zaidi

Ruwaza ya kidahizo kimoja kwa antonimu tano au zaidi hujulikana pia kama ruwaza ya utano au wingi. Licha ya neno 'uwingi' kumaanisha 'vitu zaidi ya kimoja', katika makala hii wingi ni hali ya kidahizo kimoja kutumia antonimu tano au zaidi katika ufafanuzi wake. KKK3 kama ilivyo katika lugha ya Kiswahili, yapo maneno yaliyobeba antonimu tano au zaidi. Maneno haya huwa machache zaidi ukilinganisha na yale yenye vinyume pungufu ya vitano. Kwa msingi huo, vidahizo vya ruwaza ya uwingi ni vichache katika kamusi hii. Imebainika kwamba ruwaza ya utano katika KKK3 imejitokeza pale kidahizo kimoja kilipofafanuliwa kwa kutumia antonimu tano. Kati ya vidahizo 379 vilivyoingizwa antonimu kwenye KKK3, ni vinne tu (sawa na 1.06%) vilivyotumia ruwaza ya utano. Idadi hii inaonesha uwezekano mdogo wa vidahizo vya KKK3 kuwa na vinyume vitano au zaidi katika mawasiliano ya mara kwa mara. Jedwali Na. 5 linaonesha antonimu za KKK3 katika ruwaza ya utano.

**Jedwali Na. 5: Ruwaza ya Kidahizo Kimoja kwa Antonimu Tano au Zaidi**

| Na. | Kidahizo | Antonimu 1 | Antonimu 2 | Antonimu 3 | Antonimu 4 | Antonimu 5 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | **madhila** | raha | furaha | ureda | utamu | burudani |
| 2. | **pinga** | kubali | kiri | afiki | ruhusu | ridhia |
| 3. | **udanganyifu** | ukweli | uhakika | uhakikisho | uhalisi | uthibitisho |

**Chanzo:** BAKITA (2022)

Jedwali Na. 5 linaonesha data ya ruwaza ya utano wa antonimu zilizoingizwa katika KKK3. Ruwaza hii imedhihirika kwa kidahizo kimoja kubeba antonimu tano tu na hakuna vidahizo vilivyofafanuliwa kwa antonimu zaidi ya tano. Antonimu zote zilizotumika katika ufafanuzi huwa zinahusiana moja kwa moja na kidahizo husika ilhali zenyewe kwa zenyewe zinakuwa na hali ya usawe kwa kuunda maana moja. Tuchunguze Data Na. 15 kwa ufafanuzi zaidi.

15. **pinga** **ping.a** */`piŋga/ kit.ele.* pia **pinza** **a.** kataa hoja, uamuzi, mawazo au utekelezaji wa jambo fulani unaofanywa na mtu, taasisi, shirika, chama au serikali ***vis.:*** kaidi, zuia, bishana, kanusha, kana, kinga, kinza. ***viny.:*** kubali, kiri, afiki, ruhusu, ridhia **b.** wekeana mali na mtu kimakubaliano kuwa atakayetabiri kwa usahihi k.v. matokeo ya michezo achukue mali hizo ⇌ *pingia, pingiwa, pingisha*.
**Chanzo:** BAKITA (2022: 835)

Katika Data Na. 15 antonimu zote tano zimetumika katika fahiwa ya kwanza inayohusu ‘kukataa’. Kimawasiliano, matumizi ya antonimu hizo hutakiwa yajikite kwenye ujenzi wa maana inayohusiana na fahiwa ya kwanza ya kidahizo ‘pinga’. Antonimu hizi kwa ujumla wake zimesaidia kuipambanua zaidi maana ya kidahizo ingawa zenyewe kwa zenyewe haziundi usawe ulio kamili.

Kimsingi, imebainika kwamba hakuna kidahizo chochote katika ruwaza hii kilichobeba antonimu zaidi ya tano. Hali hii inaashiria kuwa KKK3 haijaingiza antonimu zote zinazohusu kidahizo husika, hata kama kidahizo hicho huwa na sifa ya kubeba antonimu zaidi ya tano. Kwa ufafanuzi zaidi, tuchunguze Data Na. 16 inayohusu kidahizo ‘madhila’.

16. **madhila** */ma`ðila/ nm.* (*Ø*) {*ya-*} pia **madhilifu** mateso au taabu zinazomzonga mtu ***mat.:*** *Juma hana raha kwani ~ yamemsonga*. ***vis.:*** adha, maudhi, mashaka, karaha ***viny.:*** raha, furaha, ureda, utamu, burudani. **Chanzo:** BAKITA (2022: 548)

Data Na. 16 inaonesha matumizi ya antonimu tano katika ufafanuzi wa kidahizo ‘madhila’. Hata hivyo, kutokana na asili yake, kidahizo hiki kingeweza kuongezewa antonimu zingine zaidi zinazotokana na sifa ya antonimu hizo kuwa na visawe vyake. Hii ni kwa sababu baadhi ya antonimu za kidahizo husika huwa na sinonimu zake zingine nje ya zilizoingizwa katika kamusi. Kimsingi, antonimu mojamoja ikichunguzwa zaidi, kuna uwezekano wa kupatikana kwa visawe vya antonimu husika ambazo zikitumika katika ufafanuzi wa kidahizo ‘pinga’ zitaongeza zaidi antonimu zake. Kwa mfano, kidahizo ‘raha’ katika KKK3 kimeingizwa sinonimu ‘*starehe*’ na ‘*uhondo*’. Kadhalika, ‘ureda’ sinonimu yake ni ‘*anasa*’. Kuwapo kwa sinonimu hizo kungeweza kupambanua ruwaza yenye antonimu zaidi ya tano katika kidahizo husika. Kwa hiyo, ili kubeba kipengele cha antonimu zaidi ya tano, kidahizo ‘madhila’ kingeweza kufafanuliwa kwa antonimu nane ambazo ni, ‘*raha*’, ‘*furaha*’, ‘*ureda*’, ‘*utamu*’, ‘*burudani*’, ‘*starehe*’, ‘*uhondo*’ na ‘*anasa*’. Kutoingizwa kwa maneno hayo kumesababisha KKK3 iwe na ruwaza ya juu kabisa inayoishia na antonimu tano tu. Matumizi ya antonimu hizo hutofautiana katika muktadha na kusudio la maana, hivyo, mtumiaji wa Kiswahili hupaswa kuwa makini ili kutoharibu mawasiliano husika.

## 5.0 Hitimisho

Kulingana na data zilizowasilishwa imebainika kuwa ruwaza za kiidadi katika antonimu za KKK3 zimejitokeza kwa namna kuu tano. Ruwaza hizo ni umoja, uwili, utatu, unne na utano. Kati ya ruwaza hizo, ruwaza ya umoja ndiyo iliyotawala kwa 68.87% ikifuatiwa na ruwaza ya uwili kwa 24.27%, kisha ruwaza ya utatu kwa 3.43%. Nyingine ni ruwaza ya unne yenye 2.37% na ile ya utano yenye 1.06%. Pia, imebainika kuwa KKK3 imejumuisha baadhi ya vidahizo vyenye sifa za kupata antonimu kisemantiki na kileksikografia lakini havijapewa antonimu hizo. Kwa ujumla, ruwaza za kiidadi zilizojitokeza katika antonimu za KKK3 zinathibitisha utajiri na uhusiano wa maneno katika kamusi madhukura. Aidha, imebainika kuwa KKK3 ina ruwaza asili za idadi ya antonimu ambazo hutokana na sifa asilia ya kidahizo kuwa na idadi kamili ya antonimu kama zilivyojitokeza kwenye kamusi. Pia, kuna ruwaza unde za idadi ya antonimu; hizi hutokana na maamuzi ya watunga kamusi kuteua baadhi tu ya antonimu za kuingizwa katika ufafanuzi wa kidahizo. Kwa mujibu wa KKK3, ufafanuzi wa vidahizo vya kiantonimu umeonekana kutawaliwa zaidi na antonimu mojamoja. Idadi hii ni ishara kuwa unyume katika KKK3 umejikita kwenye neno mojamoja, japokuwa katika mazingira mengine hupatikana zaidi ya antonimu moja. Makala hii inapendekeza kuwekwa bayana zaidi vigezo vya kuzipangilia antonimu ndani ya ufafanuzi wa kidahizo kimoja. Vigezo hivyo vinaweza kuwa mpangilio wa kialfabeti, historia yake, mantiki au kiwango cha matumizi ya antonimu husika. Vilevile, inapotokea kidahizo kimeingiziwa sinonimu kadhaa, ni muhimu antonimu za kidahizo husika ziingizwe kwa kutegemea mfuatano na idadi ya sinonimu zinazohusika.

## Marejeleo


Barker, C. (2001). *Lexical Semantics: Encyclopedia of Cognitive Science*. San Diego: Macmillan References Ltd.

BAKITA (2022). *Kamusi Kuu ya Kiswahili (Toleo la 3).* Nairobi: Longhorn Publishers PLC.

Cruse, D.A. (1986). *Lexical Semantics*. Cambridge: Cambridge University Press.

Gao, C. na Zheng, Q. (2014). “A Linguistic Study of Antonymy in English Texts”. *Journal of Language Teaching and Research*. 5 (1): 234 - 238.

Geeraerts, D. (2010). *Theories of Lexical Semantics*. New York: Oxford University Press.

Gibbe, A. (1977). Homonymy, Synonymy and Antonymy in Kiswahili: *A Lexical Study*. Tasinifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Habwe, J. na Karanja, P. (2012). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Jackson, H. (2013). *Words and their Meaning*. London: Taylor and Francis Group.

Jones, S. (2002). *Antonym: A Corpus-based Perspective.* Amsterdam: Routledge.

Kahigi, K.K. (2019). *Misingi ya Semantiki na Pragmatiki ya Kiswahili: Kwa ajili*

*ya Vyuo na Vyuo Vikuu*. Dar es Salaam: KAUTTU.

Lobanova, A., Tom, K. na Jennifer, S. (2010). "Defining Antonymy: A Corpus-Based Study of Opposites by Lexico-Syntactic Patterns." *International Journal of Lexicography*. 23(1):19-53.

Mdee, J.S. (2010). *Nadharia na Historia ya Leksikografia*. Dar es Salaam: TUKI.

Murphy, L.M. (2003). *Semantic Relations and the Lexicon: Antonyms, Synonyms and Other Semantic Paradigms*. Cambridge: Cambridge University Press.

Paradis, C. na Willners, C. (2006). "Selecting Antonyms for Dictionary Entries: Methodological Aspects". *Working Papers*. 6: 95-106.

TUKI (2019). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu (Toleo la 4)*. Nairobi: Oxford University Press East Africa Limited.

Wiegand, H.E. (1983). "On the Structure and Contents of a General Theory of Lexicography". Katika R.K.R. Hartman (Mh.), *Lexeter Proceedings*. Tubingen: Max Verlag. Kur. 13 - 30.

Zgusta, L. (1971). *Manual of Lexicography*. The Hague: Mouton.